



**JAMHURI YA MUUNGANO WA
TANZANIA
CHUO CHA UHASIBU ARUSHA**



TANGAZO LA KOZI

**KOZI YA KUBORESHA UTENDAJI KAZI NA MAWASILIANO KWA
WAHUDUMU WA OFISI**

1.0 UTANGULIZI

Hii Kozi imeandaliwa mahususi kwa ajili ya kuleta maboresho, tija na ufanisi wa kazi kwa Wahudumu, Walinzi na Wafanya Usafi katika Taasisi wanazotumikia. Wahudumu, Walinzi na Wafanya Usafi wamekuwa kiungo muhimu katika taasisi nyingi kwa uwajibikaji wao kuweza kufikia malengo ya taasisi. Ikiwa mafunzo mafupi ni sehemu ya kuboresha kazi zao, ni mategemeo yetu kwamba baada ya kozi hii watakuwa na elimu ya ziada katika utendaji wa kazi zao za kila siku.

2.0 MALENGO YA KOZI

Mwisho wa kozi hii mshiriki atakuwa na uelewa mpana katika maeneo yafuatayo:

- (a) Muundo wa Taasisi anayofanyia kazi;
- (b) Wajibu wa Mhudumu, Mlinzi na Wafanya Usafi;
- (c) Utumiaji wa Vifaa vya Ofisi kwa njia ya Komputa;
- (d) Kupokea, kutoa na kutekeleza maagizo;
- (e) Maadili ya kazi;
- (f) Ubebaji wa nyaraka na majalada ya ofisi;
- (g) Ushirikiano na uwajibikaji;
- (h) Jinsi ya kuweka malengo ya kazi na kuyafikia;
- (i) Matumizi Mazuri ya Muda eneo la kazi;
- (j) Kukabiliana na changamoto za kazi na Teknolojia;
- (k) Huduma za masijala kwa mtandao (E- records);
- (l) Uandishi wa ripoti; na
- (m) Mahusiano bora katika ofisi.

3.0 NANI ANAPASWA KUHUDHURIA

Hii Kozi ni Maalumu kwa Wahudumu, Walinzi na Wafanya Usafi wa ofisi.

4.0 MBINU ZA UFUNDISHAJI

Kozi hii itafundishwa kwa njia mbalimbali ikiwemo ya utoaji mihadhara, majadiliano, uchunguzi kifani na njia ya vitendo ili kuboresha tija katika Taasisi.

5.0 ADA YA KOZI

Ada ya kozi itakuwa **TShs 800,000/= (Laki nane tu)** ada hii ni kwa ajili ya vitini, chai, chakula cha mchana. Malipo hayo yafanyike moja kwa moja kwenda Chuo cha Uhasibu Arusha (Institute of Accountancy Arusha), kwenye Benki Namba **014103007130 NBC, Tawi la Arusha** kwa njia ya fedha taslimu, hundi au TISS.

6.0 TAREHE NA UKUMBI WA MAFUNZO

Kozi hii itafanyika katika eneo la Chuo cha Uhasibu Arusha, Kampusi Kuu Njiro Arusha, **tarehe 04 - 08 Desemba , 2017.**

7.0 MAWASILIANO

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:

Mkurugenzi wa Kozi: Ms. Lilian Minja

E-mail lminja@iaa.ac.tz or liliannkya2@gmail.com: Cell: 0713214513 or 0767214513

Mkuu wa Idara – Ushauri wa Kitaalamu na Kozi za Kujiendeleza (Consultancy & Executive Development) - Mr. Papias Njaala

E-Mail: pnjaala@iaa.ac.tz and pnjaala@yahoo.co.uk Cell: +255 784 436 286 and +255 777 236 286

APPLY TO:

The Rector
Institute of Accountancy Arusha
P.O. BOX 2798
Arusha.
E-Mail: iaa@iaa.ac.tz